Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 237 | SAF.-RAB.I 1444 AH | OKTOBA 2022 | NUBUWWAT 1401 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Wala msifanye uharibifu katika nchi ikiisha tulia. Na Mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Bila shaka Rehema za Allah zi karibu na wafanyao hisani. (Al-A'raaf 7:57)

Jalsa Salana Ishara inayong'aa

Na **SheikhKarimuddin Shams,** Morogoro

Ishara kuu kati ya ishara juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu Jalsa salana au mkutano wa mwaka ni miongoni mwa ishara juu ya maendeleo na mafanikio ya Jamaat e Ahmadiya inayonga'a zaidi siku hadi siku.

Mkutano huu ulianzishwa kwa amri ya Allah^{swt} kwa mkono wa Hadhrat Masihe Maud^{as} mnamo 1891. Hadhrat Ahmad^{as} aliwaita wanajumuiyya kwa ajili ya kushauriana na wazee wetu waaminifu na watukufu walifika mara moja Qadian mnamo tarehe 27 Disemba 1891 na watu 75 walihudhuria kwenye mkutano huu wa siku moja. Seyidna Ahmad^{as} aliwatangazia wanajamaati baada ya mkutano huo wa siku moja kwamba kuanzia sasa mkutano huu utafanyika kila mwaka kwenye tarehe 27-28 na 29 Disemba katika makao mkuu wa Ahmadiyya hivyo mkutano huu unafanyika kila mwaka kama kawaida. Hadhrat Ahmad^{as} aliandika kwamba:

"Inafaa zipangwe siku tatu kwa mwaka kwa ajili ya mkutano ambamo, Mungu Akipenda, ndugu wote waaminio waweze kuhudhuria katika tarehe zilizopangwa, sharti wakiwa na afya na nafasi na kutokuwa na vikwazo vikubwa. Kwa maoni yangu ni bora tarehe hizo ziwe 27,28 na 29 za mwezi Disemba."

(Uamuzi wa Kimbingu uk. 81-82)



Moja ya Mkutano Mkuu wa Mwaka - Jalsa Salana unaofanyika Qadian

Mkutano huu ulianzishwa kutoka Kadian, Kijiji ambacho hakijulikana hapo awali:

کوئی نہ جانتا تھا کہ ہے قادیاں کدھر

Ila Kijiji hiki kilipata umaarufu kuupitia mkutano huu adhimu. Na kila mwaka mkutano uliendelea kufanyika Kadian hadi 1947. Baada ya mgawanyiko wa india katika nchi mbili za Pakistan na India mikutano miwili yalifanyika mjini Lahore kisha uliendelea kufanyika mjini Rabwah Pakistani kuanzia 1949. Mkutano wa mwisho ulifanika mnamo 1983 na baada ya hapo serikali ya Pakistani iliweka kikwazo na mkutano hakufanyika kwa sababu ya kutokupata ruhusa kutoka serikali ya Pakistani hadi leo.

Seyidna Ahmad^{as} alisema wakati wa kuanzishwa kwa Mkutano huo kwamba "msiuchukulie mkutano huu kuwa mkutano wa kawaida ni jambo ambalo msingi wake umewekwa na Mwenyezi Mungu kwa mkono wake kwa ajili kuisaidia haki na kulishindisha neno la haki na Mwenyezi Mungu amewaandaa watu watakaokusanyika kwa ajili yake hivi karibuni". Hadhrat Ahmad^{as} alisema kwa nguvu kubwa na kwa adhma na Jalali kwamba msidhani kuwa mambo hayo hayatawezekana hiki ni kitendo cha Mungu Mweza ambaye hakuna kinchoshindikana kwake.

NenolaMungulikatimiabara'bara na hakuna aliyeweza kuizuia kudra ya Mungu. Uahmadiyya uliendelea kusambaa duniani kota na watu wa kila kabila, ukoo na taifa waliendelea kujiunga na Uahmadiyya na idadi ya washiriki wa Mkutano huo pia iliendele kuongezeka kila mwaka. Mkutano wa mwisho uliofanyika nchini Pakistani washiriki wake walikuwa laki tatu kasa robo.

Fadhila za Allah zilianza kudhihirika kwa namna hii pia kwamba mkutano wa mwaka ulipata kuanzishwa kwenye nchi kadhaa kaba ya kupata vikwazo kule Pakistan na mti huu ulipandwa sehemu nyingi ya dunia na kukuwa na kutoa matunda yake mema yasiyohesabika. Mkutano huu ulianza kufanyika nchini Indonesia na nchini Ghana upande mwingine kisha ulianzishwa barani America na Ulaya hasa Uingereza na Ujerumani na Canada n.k. Kwa sasa mkutano huu unafanyika kwa shani na utukufu mkubwa mno kwenye nchi nyingi za dunia za mashariki na za magharibi na neno la mungu linatimia kwa namna ya ajabu sana kwamba mataifa yataungana na nidhamu hii ya Jalsa na kila watu watakunywa maji matamu ya chemchem hii.

Hadhrat khalifa mtukufu wa nne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad^{rh} alipohama Pakistan na kuhamia Uingereza basi Jalsa hiyo ilipata adhama na utukufu mkubwa mno na ukawa mkutano wa mataifa kuanzia mwaka 1884 na ulianza kufana sana mwaka hadi mwaka. Mnamo 1993 ilipoanzishwa kituo cha luninga cha Jamaat kwa jina la M.T.A. basi mkutano huu ulipanuka na kufika hadi kona zote za dunia na watu wengi Zaidi walianza kupata baraka za kushiriki kwenye jalsa hiyo kuipitia M.T.A.

Sasa anagalieni mkutano ulioanzishwa na watu 75 leo unamahudhurio ya watu mamilioni kwa sababu ya mkutano huu unafanyika kwenye kila nchi ambamo wanajamaat wapo kwa idadi kubwa kisha kwa kuipitia M.T.A. watu wa rangi mbali mbali, toafuti tofauti, na nchi mbali mbali wanashiriki humo hivyo mkutano huu ukawa kama mti uliobarikiwa unaotoa matunda yake kila siku na matawi yake yameshasamba kwenye mabara yote ya ulimwengu na maelfu ya watu huja kushiriki kwenye mkutano huu katika nchi yetu pendwa Tanzania.

Ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu wa *Mapenzi ya Mungu* baadhi ya nukuu za Mwanzilishi Mtukufu wa Jalsa hiyo.

Hadhrat Ahmad^{as} anasema akieleza lengo kuu na shabaha ya Jalsa Salana kuwa:

"Katika mkutano huo kutakuwa na shuguli za kuelezea mambo ya ukweli na ambayo ni ya lazima kwa ajili ya kuzidisha Imani na yakini na maarifa. Na vile vile kwa jamaa hao kutafanyiwa maombi maalum

Endelea uk. 2

Msikiti ndio Maskani!! uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Harambee! Wana Kenya!



Sifa zote njema ni za Allah Aliyajalia ndugu na Jirani zetu wa Jamhuri ya Kenya kuwa na uchaguzi ambao Rais wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan amesema "ni zawadi kwa wana Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla!". Uchaguzi huu umeliletea heshima bara la Afrika na tumewafumba mdomo ambao daima wanatarajia na kushangilia mabaya yanayotoka Afrika. Ambapo ukichunguza kwa makini wao ni chanzo na chimbuko. Wakenya wamethibitisha kuwa mgawaji wa akili kwa binadamu wote ni sawa na sio kama inavyosemwa katika riwaya ya George Orwell, *Shamba la Wanyama*; "Wanyama wengine ni bora kuliko wengine".

Tutakuwa watu wa mwisho kusema kuwa uchaguzi huo umekamilika, hauna dosari, la hasha! Walioongoza na kusimamia uchaguzi huo hawakuwa Malaika walikuwa binadamu na Allah Anasema “binadamu ni dhaifu”. Licha ya ukweli huo yapo mambo ya msingi ambayo tunaweza kujifunza kutoka uchaguzi huo wa Kenya.

Hatukusikia jina la mgombea yeyote kukatwa kwa kisingizio cha aina yoyote ile.

Kumbe ushindi katika uchaguzi ni kwa nchi na sio kwa chama au mtu. *Azimio, Kenya Kwanza* havina thamani kuliko Kenya. Mwana wa Simon na mwana wa Jaramogi sio bora kuliko Kenya. Kenya ilikuwepo na itakuwepo. Sina uhakika wa hivyo viwili tulivyotaja, yaani Azimio na Kenya Kwanza.

Mwanadamu ameumbwa na wasiwasi wasiwasi hiyo inaondolewa kwa mambo kuwa wazi. Kenya mambo yalikuwa wazi. Ni uwazi wa namna hiyo unaohitajiwa na Mama Afrika.



Jalsa Salana

Ishara Inayong'aa

Kutoka uk. 1



Moja ya Mkutano wa mwaka - Jalsa Salana, wa Jumuiya ya Wasilam Waahmadiyya Tanzania

na mwelekeo mahsusi na itafanyawa bidi saw ana uwezo mbele ya Mungu Mrehemevu kwamba Mwenyezi mungu Awavutie Kwake, na Awakubalie Kwake, na Awapatie mabadilikomema.” (Uamuzi wa Kimbingu Uk;82)

Hadhrat Ahmad[as] alisema akieleza umuhimu wa kushiriki katika Jalsa na kusisitiza kuja kwenye mkutano huu hasa wale wanaokuwa na hali ndogo ya kiuchumi kwamba:

“Na itafaa kwa watu wenye uwezo mdogo kuwa waanze mapema kufikiria njia ya kushiriki katika mkutano huo. Na kama kwa ajili ya gharama ya safari ya mkutano huu ndugu waanze kujiwekea pesa kidogo kodogo pembeni kila siku au kila mwezi, bila shida pesa kwa ajili ya safari itapatikana kana kwamba safari hii itakuwa bure.”(Uamuzi wa Kimbingu Uk.83.)

Nasaha kwa wale wanaohudhuria Jalsa

Hadhrat Aqdas Masihe Maud[as]. anasem kwa uchungu wa moyoni akitunasihi kwamba:

“Nasema kweli kabisa kuwa Imani ya mtu haiwezi kuwa sawa mpaka awe ametanguliza, awezavyo, raha ya nguguye juu ya raha yake. Kama ndugu yangu mbele yangu analala chini ilhali yu dhaifu na mgonjwa, nami juu ya kuwa mwenye siha na afya nakitwaa kitanda ili huyu asipate kujikalia hicho ,basi ni masikitiko kwa hali yangu kama nisiinuke na nisimpe kitanda changu kwa mahaba na huruma wala nisijipendelee kulala chini. Kama ndugu yangu ni mgonjwa na hajiwezi ,basi ni masikitiko kwa hali yangu kama mbele yake nilale kwa amani na nisimtafutie njia ya kumpatia raha sawa na uwezo wangu. Na kama ndugu yangu katika dini anitolee ukali kidogo kwa kiburi, basi ni masikitiko kwa hali yangu kama nimtendee vikali maksudi, bali yanipasa nivumilie maneno yake na kumwombea katika sala zangu kwa uchungu, kwani yu ndugu yangu na anaugua kiroho. Kama ndugu yangu ni punguani au hana ujuzi au kwa kupungukiwa busara apate kukosea, basi haifai nimdhihaki au kukunja kipaji na kumtolea ukali na kumwaibisha, kwani hizo zote ni njia za kuangamiza. Mtu hawezi kuwa mwaminio wa kweli maadamu si mpole wa moyo na hajioni duni kuliko wote, na majivuno yote hayatoweki. Kuwa hadimu wa kaumu ndio alama ya kuwa Bwana. Kuongea na wenye hali ndogo kwa upole na unyenyekevu ni alama ya kukubaliwa na Mungu, na kutoa jawabu la maovu kwa mema ni alama za bahati njema. Kuzuia ghadhabu na kuvumilia maneno makali ni ushujaa wa daraja ya juu. Lakini naona mambo hayo hayamo ndani ya baadhi ya wanajumuiyya wangu.” (Ushahidi wa Kurani uk.214-215)

Maombi ya Hadhrat Ahmad[as] kwa Washiriki

Huzur anasema:

“Ndugu wote waliohudhuria kwa kuvumilia shida za safari kwa ajili ya Mungu tu, Mwenyezi Mungu Awalipe malipo mema na Awajaalie thawabu ya kila hatua waliochukua. Amin Allahumma Amin.” (Uamuzi wa Kimbingu 83-84)

Bwana wetu mpendwa mtume Muhammad saw alitoa bishara kwa ajili ya walewanaokusanyikakwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwamaba wale watu wanaokaa Pamoja na kumkumbuka Allah wanapata msamaha wa madhambi yao na kuingizwa kwenye pepo ya Mola wao hivyo tuje kwa shauku na jazba kwa ajili ya kushiriki kwenye Jalsa hiyo itakayofanyika mwaka huu mjini Dar-es-Salam. Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kufika kwa wingi na tupate baraka za kila namna za mkutano huu. Aamina.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Lajna Imaillah na Nasratul Ahmadiya Wafanya Ijtimai Yao ya Kitaifa kwa Mafanikio Makubwa katika Viwanja vya Jamaat Kitonga Dar es Salaam

Na Idara ya Ishaat
Lajna Imaillah Tanzania

Mnamo tarehe 12 na 13 mwezi Agosti 2022 Tandhim ya Lajna Imaillah Tanzania imefanikiwa kufanya Ijtimai yake ya kitaifa kwa mafanikio makubwa katika Viwanja vya Jamaat vilivyopo Kitonga Jijini Dar es Salaam, ikifuatiwa na mkutano wa shura ya kitaifa uliofanyika tarehe 14 Agosti 2022. Ijtimai hii imefanyika mara baada ya kuahirishwa mara mbili tangu mwaka 2019 kutokana na athari za UVIKO 19 ulioikumba dunia kwa ujumla. Jumla ya washiriki 789 kutoka matawi 77 na mikoa 16 nchini walihudhuria kwenye ijtmai hii ambapo lajna walikuwa 507, Nasrat 238 na Atfal 44. Alhamdulillah.

Ijtimai ilifunguliwa kwa usomaji wa Qur an Tukufu iliyosomwa na Bi Maimuna Mbambwa kutoka tawi la Kingugi na kisha Sadr Lajna Taifa Bi Zanana Omary aliongoza kiapo cha Lajna Imaillah. Mkutano huu ulifunguliwa kwa mashairi mawili, la kwanza ni Shairi la Masihi aliyeahidiwa a.s lililosomwa na Majlis Lajna Imaillah Taifa na kisha shairi la ufunguzi lilisomwa na Bi Zamda Mbungiro kutoka Tawi la Kitanga.

Hotuba ya ufunguzi ilitolewa na Mwalimu Ally Rashid Sahib kwa niaba ya Amir Sahib. Mwalimu Sahib aliwaasaa lajna na nasirat wote kuzingatia lengo kuu la mkutano huo kuwa ni kwa ajili ya kujijenga kiimani na kielimu zaidi. Hivyo, wanapaswa kushiriki kikamilifu kwenye kila shindano lililoandaliwa. Kisha Ijtimai ilifunguliwa kwa maombi ya kimya kimya yaliongozwa na Mwalimu Sahib.

Mara baada ya Ijtimai kufunguliwa Sadr Lajna Taifa Bi Zanana Omary alitoa nasaha fupi kuhusu malezi ya watoto kutokana na hali halisi ya kimalezi ilivyo kwa jamii yetu na ukizingatia kuwa tulikaa muda mrefu bila ya kuwa na Ijtimaa.

Kisha ijtimaa ilianza kwa Mashindano ya kielimu ya kuhifadhi Quran Tukufu bila tafsiri na tafsiri, Usomaji wa Quran Tukufu, maswali na majibu, sambamba na usomaji wa hutoba kwa Lajna na Nasrat. Mashindano yalifanyika kwa mafanikio makubwa. Baada ya mashindano haya ya kielimu kuisha Naib Sadr Lajna Taifa Bi Zena Nyange kwa niaba ya Sadr Lajna Taifa alifanya uzinduzi wa kijarida cha Lajna Imaillah Tanzania cha AN-NUSRAT ambacho jina lake limetolewa na Khalifatul masih V atba chenye lengo la kukuza uelewa wa Lajna na Nasrat kwenye masuala mbalimbali ya Tandhim, Jamaat na jamii kwa ujumla Siku ya jumamosi lajna na Nasrat waliohudhuria kwenye ijtmaa hii walielekea uwanjani kwa ajili ya kushiriki michezo mbali mbali kama vile mpira wa miguu, kuvuta kamba kwa wanene na wembamba, kuendesha baiskeli, kutunga uzi kwa wazee, kukimbia kwenye gunia, kukimbia na ndimu kwenye kijiko, kufikisha kauli pamoja na kukalia puto. Mwisho wa mashindano yote hayo washiriki walikabidhiwa zawadi na Sadr Lajna Taifa Bi Zanana Omary kadhalika nasaha mbalimbali zilitolewa kwa washiriki wa mashindano ya kielimu hasa kuboresha Usomaji wa Quran tukufu.

Hotuba ya kufunga Ijtimai ilisomwa na Kaimu Amir Sahib ambaye pia ni Naibu Amir Sheikh Abdurahman Ame Sahib. Katika hotuba hiyo aliwakumbusha washiriki kuwa Tandhim ya kwanza kuanzishwa ni Lajna Imaillah na kuwa sio Tandhim changa na kimsingi mwaka huu inatimiza miaka mia moja (100). Hivyo wanapaswa kuwa mstari wa mbele kwenye kutekeleza mipango yao wenyewe ili kutimiza lengo la kuanzishwa kwake. Pia alikumbusha jukumu la kuandaa hutoba ni lao wenyewe hivyo wajitahidi kusoma wenyewe ndio itasaidia kukuza uwezo wao wa kielimu na sio kuwategemea kina baba. Kadhalika alisema kuwa tarehe iliyowekwa katika kijarida hicho imekosewa ilipaswa kuwa kwa mwaka na sio tarehe iliyoandikwa na kwamba ni makosa ya kiufundi. Hata hivyo, alipendekeza kuwa kutokana na okongwe wa Tandhim ya Lajna Imaillah kijarida chake kilipaswa kutolewa walau mara tatu kwa mwaka. Kisha Ijtimai ilifungwa kwa maombi ya kimya kimya yalioongozwa na Kaimu Amiri Sahib.

Siku ya Jumapili ilikuwa ni shura ya kitaifa ambapo ajenda tatu zilijadiliwa. Ajenda ya kwanza ni yamalezi ambapo ilikuwa inasema “Nini kifanyike kwa Lajna ili waweze kutekeleza ipasavyo malezi ya watoto”. Ajenda ya pili ilikuwa bajeti pendekezwa ya mwaka 2022-2023 na nini kifanyike ili Lajna na Nasrat waweze kutoa michango yao kwa wakati ili kutimiza bajeti kwa asilimia 100. Ajenda ya tatu ilikua ni uchaguzi wa sadri lajna taifa, Mwisho sadri lajna aliwaaombea washiriki wote warudi majumbani salama na kwenda kuyatekeleza yote waliojifunza

Hata hivyo, kwa fadhili za Allah katibu wa Waqfu Nau Taifa Bwana Amir Kaluta alipata nafasi ya kuwakumbusha Lajna kuhusu kuwatoa watoto wao waqfu kwa ajili ya kuitumikia jamaat. Alisema jukumu hili ni letu hasa. Hivyo tufanye maombi kwa Allah wakati wa kulitekeleza pia tujitahidi watoto wetu ambao tumewatoa katika njia ya Mwenyezi Mungu tuweze kuwalea sawa na maagizo yanayotolewa na muongozo wa waqfu nau.

Kwa Fadhili za Allah mpaka Makala hii inachapishwa majibu ya ripoti ya Ijtimai na shura ilikuwa imekwisha jibiwa na Khalifatul Masih V atba na kuwa Hudhur Aqdas ameridhia mapenekezo yote ya shura yaliyopendekezwa. Pia amemuidhinisha Bi Zena Nyange Sahiba kuwa Sadr Lajna Imaillah Tanzania kwa kipindi cha 2022-2024 mara baada ya Bi Zanana Omary Sahiba kumaliza muda wake. Kisha Khalifatul Masih V atba aliiombea dua Tandhim ya Lajna Imaillah Tanzania kuwa Allah sw aiwezeshe katika kutimiza vyema malengo yake iliyojiwekea na kuwa Allah sw awazidishie juhudi yao katika kuitumikia dini. Amin.

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad^{ra} Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa^{as}

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

UKOROFI MPYA TOKA KWA WATU WA MAKKA

Kama vile imevyokwisha elezwa kwamba baada ya miezi miwili mitatu hivi, wakati hofu ilipowaondoka watu wa Makka, basi wakaanzisha tena matayarisho dhidi ya Islam. Hivyo ndani ya siku hizo hizo, Kiongozi fulani wa Madina, Saad bin Muadh, aliyekuwa kiongozi wa kabila la Aus, alienda Makka kwa ajili ya kutufu nyumba ya Mwenyezi Mungu (Kaaba). Abu Jahal alipomuaona, akamwambia kwa hasira: Je ninyi watu mnadhania hivi kwamba baada ya kumpa hifadhi mritadi yule (Muhammad s.a.w.) mtaweza kuitufu kaaba kwa amani? Nanyi mnadhani kwamba mnao uwezo wa kumhifadhi na kumsaidia? Kwa haki ya Mwenyezi Mungu, kama wakati huu isingekuwa kwa ajili ya Abu Safwan, basi usingeweza kusalimika na kwenda kwa watu wa nyumbani kwako. Saad bin Muadh akasema: Wallaahi, kama ninyi mtatuzuia tusije kwenye Kaaba, basi kumbukeni kwamba nanyi pia hamtapata amani kwenye njia yenu ya kuendea Sham.

Ndani ya siku hizo hizo, Walid bin Mughira, kiongozi fulani mkubwa wa Makka aliumwa na akahisi kwamba mauti yake yakaribia. Siku moja viongozi wakubwa wa Makka walikuwa kwake, basi akashindwa kujizuia na akaanza kulia. Viongozi wa Makka wakashangaa na kumuuliza hivi kwa nini unalia? Walid akasema: Je mnadhani ya kwamba mimi nalia kwa kuhofia mauti? Wallahi si hivyo hata kidogo. Huzuni yangu ni hii kwamba isje dini ya Muhammad ikaenea na hata Makka nayo ikawa chini ya himaya yake. Abu Sufian akajibu kwa kusema: Usilihuzunikie jambo hili. Hilo halitokuwepo maadam tuko hai. Sisi tunatoa dhamana ya jambo hili.

Kutokana na matukio yote haya yathibitika kwamba muhula ule uliopatikana wa kutokuwepo kwa dhulma toka kwa watu wa Makka ulikuwa ni wa muda tu. Watu walikuwa wakihamasishwa tena. Viongozi waliokuwa wakikaribia kufa walikuwa wakiwalisha watu viapo vya kumpinga mtume wa Mungu Muhammad s.a.w. wakati wakiwa katika vitanda vyao vya mauti. Watu wa Madina walikuwa wakitayarishwa kumpinga Muhammad s.a.w. katika njia ya vita na mashinikizo yalikuwa yakitumika dhidi ya wenye kukataa kwa kuwaambia kwamba watu wa Makka pamwe na makabila yaliyo na mikataba nayo ya ushirikiano wataishambulia Madina na kuwaua wanaume wa Madina na kuwafanya watumwa wanawake.

MIPANGO YA KUJIHAMI YA MTUME S.A.W.

Hivyo, kama katika hali hizi, Mtume s.a.w. angejikalia kimya huko Madina na kutofanya matayarisho yoyote ya kuilinda Madina, basi kwa yakini angepata lawama kubwa sana. Hivyo akaanza kuwatuma masahaba zake kwa sura ya vikundi vidogo vidogo pembezoni mwa Makka ili awe na taarifa ya harakati za watu wa Makka. Wakati mwingine watu hawa wa vikundi hivi walikuwa pia wakikabiliana na baadhi ya misafara ya watu wa Makka au baadhi ya makundi fulani fulani ya watu wa Makka. Na baada ya kuonana kukawa na hali ya kukaribia kabisa kupigana.

Waandishi wa Kikristo wanaandika kwamba huo ulikuwa ni uchokozi uliofanywa na mtume wa Mungu Muhammad s.a.w. Je dhulma ile iliyofanywa dhidi ya Waislamu huko Makka kwa miaka kumi na tatu mfululizo na juhudi zile zilizofanywa za kuwahamasisha watu wa Madina dhidi ya Waislamu na kisha vitisho vile vilivyofanywa vya kuishambulia Madina, je yaweza kusemwa kwamba huo ulikuwa ni uchokozi kwa kupeleka vikundi vya watu kwa ajili ya kupata taarifa za kujihami?

Ni kanuni ipi ya dunia, ambayo hata baada ya dhulma za huko Makka za miaka kumi na tatu, inayofahamu kuwa kunahitajika sababu zaidi ya kuchochea vita kati ya Waislamu na watu wa Makka? Leo nchi za Magharibi zinajidhani kuwa ndizo zilizostaarabika kuliko zote. Yale yaliyotokea huko Makka, kama nchi yoyote ile ipigane vita kutokana na nusu tu ya yale yaliyotokea Makka, kuna mtu yeyote awezaye kuisema nchi hiyo kuwa ina hatia?

Je kama kuna serikali yoyote inawalazimisha watu wa nchi nyingine kuwaua kundi la watu fulani au kuwafukuza kutoka nchini kwao, je kundi hili (linalodhulumiwa) linakuwa halina haki ya kutangaza vita dhidi yake (hiyo serikali)? Hivyo baada ya kustawi kwa serikali ya Kiislamu huko Madina, kulikuwa hakuna haja nyingine yoyote mpya kutokea. Matukio ya maisha ya kule Makka yalikuwa yakiwapa Waislamu haki kamili ya kutangaza vita dhidi ya watu wa Makka. Lakini mtume wa Allah, Muhammad s.a.w. hakufanya hivyo. Alifanya subira na akazidhibiti juhudi zake katika kuufahamu tu utukutu wa maadui.

Lakini wakati watu wa Makka wenyewe walipoanza kuwashawishi watu wa Madini dhidi ya Waislamu, wakawazuia Waislamu kwenda kuhiji, misafara yao (watu wa Makka) iliyokuwa ikienda Syria ikaacha kutumia njia zao za asili na kuanza kupitia kwenye njia za makabila yaliyokuwa yameizunguka Madina na kuanza kuwachochea dhidi ya watu wa Madina, hivyo kwa ajili ya kuihami Madina Waislamu nao pia walilazimika kuikubali changamoto hiyo ya vita iliyokuwa ikitolewa na watu wa Makka kwa miaka kumi na nne mfululizo. Na hakuna mtu yeyote duniani mwenye haki ya kulaumu kukubali huko kwa changamoto hiyo.

MSINGI WA SERIKALI YA KIISLAMU HUKO MADINA

Pale Mtume s.a.w. alipokuwa akipeleleza hali za nje, hakuwa pia ameghafilika kuirekebisha hali ya Madina. Imekwisha elezwa kwamba washirikina wa Madina, wengi wao walikuwa wameshasilimu kihalisia na baadhi yao kinafiki. Ndio sababu Mtume s.a.w. akawaanzishia mfumo wa serikali ya Kiislamu. Kwanza, sawa na desturi za Kiarabu, watu walikuwa wakifanya uamuzi wa kuzipata haki zao kwa kupigana vita. Sasa makadhi wakawa wameteuliwa rasmi ambao hakuna mtu yeyote aliyeweza kuipata haki yake kutoka kwa mwingine bila ya uamuzi wao.

Mwanzoni watu wa Madina hawakuwa na muelekeo kwenye elimu. sasa ukafanywa mpango huu kwamba wasomi waanze kuwaelimisha wasiokuwa na elimu. Dhulma, ukatili na ukosefu wa haki vikazuiliwa. Haki za wanawake zikastawishwa. Sawa na sheria, kodi ikapangwa kwa wote waliokuwa na mali iliyokuwa ikitumiwa kwa masikini na iliyokuwa pia ikitumiwa kwa ajili ya kuuendeleza mji. Haki za wafanyakazi zikalindwa. Mipango ya kudumu ikafanywa ya kuwaelimisha wale wasiokuwa na mbele wala nyuma. Biashara ikalazimishwa kuwa ndani ya maandiko na ndani ya mikataba. Ukatili dhidi ya watumwa ukazuiwa. Mkazo ukawekwa kwenye usafi na kwenye kulinda afya. Sensa ikaanzishwa. Hukumu zikatolewa za kuipanua mitaa. Hukumu zikatolewa za kuziweka barabara katika hali za usafi. Kwa uchache kanuni zote za kifamilia na za kijamii zakatungwa na mipango ikafanywa ya kuzidumisha. Na kwa mara ya kwanza, Waarabu wakazifahamu desturi za jamii iliyostaarabika na kunadhimika. Hapa Mtume s.a.w. alikuwa akitoa kanuni ya aina hii kwa Waarabu iliyokuwa iwe sababu ya heshima, hadhi, amani na maendeleo, sio tu kwa ajili ya zama hizo, bali kwa ajili ya zama zote kwa ajili yao na kwa ajili ya watu wengine duniani. Kule, watu wa Makka walikuwa daima wakijishughulisha kufanya maandalizi ya kivita dhidi ya Waislamu, ambayo matokeo yake yakadhihirika katika sura ya vita vya Badri.

Itaendelea toleo lijalo

Hadhrat Ahmad[as] na Wapinzani

Na **Abu Dani Shams**

Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiyya ya waislamu waahmadiyya Seyidna Ahmad[as] , Masihi na Mahdi aliyeahidiwa akiwapa tambio wapinzani wake na maadui zake alisema " *nyinyi hamwezi kunitolea aibu yoyote au uzushi au uwongo au udanganyifu kutoka katika maisha yangu ya awali ili muwaze hivi kwamba yule mtu ambaye tangu mwanzo ni mwenye mazoea ya kusema uwongo na uzushi hapo pia atakuwa amesema uwongo. Nani miongoni mwenu awezaye kunitolea lawama yoyote ile katika maisha yangu? Basi hii ni fadhili ya Mwenyezi Mungu Ambaye toka awali Amenistawisha katika ucha Mungu na hii ni dalili kwa wenye kufikiri.*" (Tadhkiratu Shahadataene Ukurasa 62)

Wasomaji watukufu wa "*Mapenzi Ya Mungu*" huu ndio ukweli usiofichika kwamba tangu Seyyedna Ahmad a.s. aliwaita wapinzani na maadui zake zaidi ya karne imepita lakina hakuna awezaye kuvunja kauli yake hiyo hadi siku ya kupigwa kwa baragumu, bali siku hadi siku wanaendelea kuthibitisha ukweli wa mshuja huyu adhimu wa Mwenyezi Mungu aliyetumwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuwakusanya watu wote chini ya bendera ya Umoja wa Mwenyezi Mungu. Waarabu wanasema:

"وَالْفَضْلُ مَا شَهِدَتْ بِهِ الاَ عْدَاءُ" yaani fadhila na ubora ndio ule unaotolewa maadui.

Hivyo basi ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu baadhi ya ushuhuda wa wapinzani ili wapate kujua cheo kilichsifika cha hazrat Ahmad a.s.

Daraja la kuonewa Wivu... na hana doa lolote

Mwanachuoni mashuhuri wa kidini wa India , mfasiri wa Qurani na mwandishi wa habari, Bwana Abu ul Kalaam Azaad akitoa ushahidi wake



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmadas
Masihi na Mahdi aliyeahidiwa

alisema "*Hakuna doa lolote liwalo linaloonekana kwenye tabia na khulka za Mirza Sahib. Yeye aliishi jinsi aishivyo mtu mwema na akapitisha maisha yake kama mcha Mungu. Kwa neno zima, miaka hamsini za mwanzo za maisha yake, kutokana na khulka na tabia zake njema na huduma zake na utetezi wake wa dini ya Kiislamu, zikampandisha kwenye daraja la juu lililotukuka na linalostahili kuonewa wivu miongoni mwa waislamu.*"

(Akhbaar Wakeel Amratsar 30 May 1908)

Mwenye kumfuata Mwenyezi Mungu

Hadhrat Qutbul Auliyaa , Abuu Is'haq Ibrahim bin Sheher Yaar r.a. , aliyekuwa walii na mwanazuoni mkubwa wa Kiislam alisema: "*Yule mtu anayemtii Mwenyezi Mungu katika ujana wake basi hata katika uzee atakuwa ni mwenye kumfuata Mwenyezi Mungu.*"

Mkweli... Mwenye kufuata sheria ya Mtume[saw]

Mwanazuoni maarufu wa dhehebu la Ahl Hadithi, aitwaye Maulvi Muhammad Husain wa Batala (kiongozi mkuu wa dhehebu lake na Mhariri wa gazeti lake) akitoa maoni yake juu ya kitabu cha Seyidna Ahmad[as] kiitwacho *Baraaheen e Ahmadiyya* aliandika katika gazeti lake liitwalo "*Isha'atu Sunna*" Mtungaji wa kitabu cha Baraheen e Ahmadiyya, kwa ushuhuda na uzoefu wa watu wanaomwafiki na wale wampingao, ni mtu mkweli, mcha Mungu na mwenye kufuata sheria ya Mtume Muhammad[saw]. (Ishaat Sunna, Jalada la 7, Ukurasa 9)

Baba mpendwa wa kiongozi maarufu wa Kiislamu, mwandishi wa habari na mshairi, Bwana Zafar Ali Khan, Munshi Sirajud Deen, mhariri wa gazeti la *Zameendaar* akitoa ushuhuda wake alisema "*Sisi twaweza kusema kwa ushuhuda wa kujionea kwa macho kwamba (yeye) alikuwa ni mtu mwema na mcha Mungu hata katika ujana wake. Yeye alijiweka mbali na udanganyifu na uzushi.*"
(Akhbaar Zameendaar May)

Mwenye kuleta Mapinduzi....na fahari ya wanadamu

Maulana Abu ul Kalaam Azaad aliandika katika gazeti lake liitwalo *Wakiil* baada ya kufariki kwa Hazrat Ahmad[as] kuwa: "*Huyo bwana, mtu maarufu ambaye kalamu yake ilikuwa ni muujiza mtupu na hotuba zake zenye mvuto wa ajabu, mtu aliyekuwa na maajabu ya ubongo ambaye kukutizama kwake kuliweza kukuteka na ambaye sauti yake ilikuwa ni wito kwenye ufufuo, ambaye vidole vyake vilikuwa vimeshika nyaya za mapinduzi na ambaye mikono yake ilibeba betri zilizo tayari za umeme, bwana huyu ambaye kwa miaka thelathini alisababisha matetemeko na dhoruba katika ulimwengu wa dini, ambaye alikuwa kama mpiga baragumu la siku ya miwsho, akaendelea kuwaamsha wale waliozama katika mambo ya dunia. Kifo cha Mirza Ghulam Ahmad Sahib wa Qadian ni kifo ambacho mtu hawezi kukosa somo na kuacha tu kifo hicho kitiririke katika mkondo wa historia na ukajiridhisha. Watu wanaoleta mapinduzi katika ulimwengu wa kiroho na kisomi hutokea kwa nadra, watoto hawa maarufu wa historia, fahari ya binadamu hawafiki mara kwa mara na pindi watokeapo hawaondoki duniani hadi wameleta mapinduzi.*"
(Wakil, Amristar, (Tarikh-e-Ahmadiyyat, Jal. 2, uk. 560).

Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kumfuata bara'bara Ashiqi huyu wa Mtume mtukufu[saw]. Aamin!

Bustani ya Washairi

AHMADIYYA NA MAENDELEO YA KISWAHILI – TANZANIA

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Mama wa waaminio

138. Habari zikaenea,
Kila pembe kusambaa,
Hadija kazisikia,
Mama huyo wa ulua.

139. Mti unajulikana,
Matunda utayaona,
Tena ya kila namna
Mtini kujichumia.

140. Mama aliyesifika,
Utajiri kadhalika,
Katika mji wa Maka,
Sifaze zilienea.

141. Binti Huwailadi,
Katika yake fuadi,
Karidhika Muhammad*saw*,
Waweze kufunga ndoa.

142. Kaongoza msafara,
Kwa hekima na busara,
Shahidi ni Marisara,
Kwa Hadija katongoa.

143. Kaeleza kwa makini,
Mwenendo wake amini,
Kama ua la uzani,
Sifa kummiminia.

144. Hadija akapeleka,
Ujumbe ukamfika,
Nikahi ikafungika,
Pasipo na kuchelea.

145. Kidogo turudi nyuma,
Maisha yawe tumama,
Tuweze kuja tizama,
Nyuma alikotokea.

146. Mama yetu ashirafu,
Mama yetu mtukufu,
Wa mbele katika safu,
Na dini kusaidia.

147. Mama yetu ni Hadija,
Ndiye mama mwenye tija,
Kampa kubwa faraja,
Rasuli akatulia.

148. Akianda masurufu,
Kwa ile safari ndefu,
Kwenye pango maarufu,
Apate mcha Jalia.

149. Siku hiyo akarudi,
Huku anayo baridi,
Nifunike binti sudi,
Baridi nanisikia.

150. Nini kilichokupata,
Dawa tupate tafuta,
Tutoe huu utata,
Nyumbani uloingia.

151. Akaanza mahubiri,
Kuwapa watu habari,
Zitokazo kwa Kahari,
Wasije kuteketea.

152. Ilikuwa patashika,
Ikamfika shabuka,
Adui wakafumuka,
Maovu kumtendea.

153. Mji wa Maka kahama,
Kuiepuka zahama,
Kaenda mji wa neema,
Madina inayong'aa.

154. Kafanya uadilifu,
Katiba ile tukufu,
Kaifata bila hofu,
Na haki ikaenea.

155. Kasahau ya zamani,
Walomtenda amini,
Yalopita tuzikeni,
Si ndwele yalotokea.

156. Somo hilo bulibuli,
Katuachia Rasuli,
Kusamehe ni asali,
Ndio dawa asilia.

157. Ni wengi wakavutika,
Makundi kumiminika,
Ili wapate baraka,
Kwenye maji ya afia.

158. Tizama wahangaika,
Watu wameweweseka,
Ni maji yamekauka,
Tone halikubakia.

159. Sauti yenye huruma,
Yawaitia uzima,
Njooni penye kisima,
Kiu mpate ondoa.

160. Kilichobaki kisima,
Chenye maji ya uzima,
Nawaona himahima,
Kiu waje iondoa.

161. Kisima chake ajabu,
Anakilinda Wahabu,
Kisimache mahababu,
Mtume wake Jalia.

162. Ni kisima cha dawamu,
Kwa ajili ya binadamu,
Ni abadi kinadumu,
Watu kuwatumikia.

163. Vyombo wamejitwalia,
Ili waweze chukua,
Maji ya kuwafalia,
Mabaya kuyaachia.

164. Kiu hino ya kiroho,
Kwake wakenda hoho,
Kufuata wa majoho,
Wale waliopotea.

165. Ibada zao ni moto,
Na vingine vyenye joto,
Majiwe hata kokoto,
Hivyo walisujudia.

166. Jua waliliabudu,
Na hata hawa wadudu,
Wakaifanya sujudu,
Vitu kuvisujudia.

167. Maasi yalishitadi,
Ikawa kwao ni jadi,
Kila siku walizidi,
Shimoni kutumbukia.

168. Maasi bara na pwani,
Wakamuenga shetani,
Kila siku maasini,
Maovu kukumbatia.

169. Haraka tena haraka,
Kisimani wakafika,
Kiu yao kukatika,
Maji hayo kujinywea.

170. Maji hayo muujiza,
Watu yakawageuza,
Mazuri wakahimiza,
Na mabaya kuachia.

Utaendelea toleo Lijalo

HOFU

1. Penzi kweli ni hofu
Hofu kumpoteza
Akili nayemwaza
Utahofu mkwaza.

2. Penzi kweli ni hofu
Hofu mkasirisha
Huzuni kumvisha
Amani kuondosha.

3. Penzi kweli ni hofu
Hofu ya kuachika
Mbali ukatengeka
Penzi likavunjika.

4. Penzi kweli ni hofu
Wema umtendee
Zidi mpendelee
Nafsi yake iteke.

5. Allah ni wakumwofu
Penzile tegemea
Dhambi takuondoa
Baraka takutia.

6. Shetani usimwofu
Hana nguvu shetani
Naye hofu rabani
Tamtia Motoni.

7. Mchawi usimwofu
Muongo takuponza
Ndugu tawakwaruza
Akili kugeuza.

8. Majini usihofu
Ujanja wawaganga
Watisha takukinga
Irizi kukufunga.

9. Jambazi usihofu
Hofu kwako rabana
Huna la wezekana
Ruhusa maulana.

10. Mola wako muhofu
Mwenye nguvu uwezo
Adhabuze ni funzo
Kuondoa uwozo.

11. Mwenyezi kimuhofu
Wema utaupenda
Naye atakupenda
Daraja utapanda.

Masihi Omary
Stambuli Kisagwa

Ahmadiyya Ukombozi duniani

1. Kwa jina lako Jalia, Wa rehma na amani
Sisi umetujaalia, Masihi kumuamini
Hali hii kufikia, kwetu nyingi shukurani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

2. Limetufikia jua, sasa hatuko gizani
Twaitwa Waahmadiyya, kwenye yakini ya dini
Wenzetu walobakia, bado wana mtihani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

3. Shime tuoneshe njia, jitihada tufanyeni,
Mafunzo ya Jumuiya, kwa dhati tuyashikeni,
Kila kwenye familia, nidhamu hii jengeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

4. Kwa kuwa twajivunia, hili ni kundi makini
Tuhubiri Jumuiya, bila ya hofu moyoni
Juhudi inatakiwa, kuimarisha imani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

5. Wapinzani wanalia, kila pembe duniani
Kuishinda Ahmadiyya, hilo haliwezekani
Kwao kilichobakia, kudumisha upinzani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

6. Allah Uliyetimia, Ituzidishie imani
Tuishike hii njia, yenye ukweli wa dini
Ingawa wanaumia, wote walio pembeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

7. Hawa wanakusudia, kutaka kuvuruga dini
Ukweli ukitakiwa, wala haufichikani
Kila yanayotakiwa, wanayaweka pembeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

8. Tabia zao za mila, wanachanganya na dini
Kubwa ya kwao dhamira, maslahi duniani
Wanafanya kila hila, kuivuruga imani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

9. Mkombozi kaingia, ndugu zetu waambieni
Wajiunge Ahmadiyya, kwenye Adili ya dini
Kama watapuuzia, mwisho wao mashakani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

10. waliopotea njia, na tuwakaribisheni
Hima wapate ingia, kabla kalantini
Wasije wakajutia, geti likipigwa pini
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

11. Tuliyo Waahmadiyya, raha, furaha moyoni
Wa nje ya Ahmadiyya, aibu misikitini
Wanadili na Dunia, sio sana ya kidini
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

12. Kalam naachia, kazi kwetu waumini
Tuhubiri jumuiya, tunusuru hii dini
Tutafute kila njia, za busara na amani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

Kassim Mohamed Mlekeni,
Ikwiriri, Rufiji, Pwani

STARA

1. Bisimilahi Rabuka, busara unijazie
Ili nisijeropoka, wakajanisema mie
Kwa kweli ninakereka, acheni nigugumie
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

2. Wadada na kina Mama, mniazime sikio
Muda wangu wa kusema, ukuninunia kwio!
Nyie ni watu wazima, ni hapana au ndio?
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

3. Funika vifua vyenu, achaneni na fasheni
Nyie wote sie wenu, tawafata majumbani
Midomo isiwe benu, tafikiri huna dini
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

4. Miguo imekubana, mwendo haueleweki
Na sisi kama vijana, twakuona husomeki
Ungevaa zile pana, tungesema chuma hiki
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

5. Na mitandio mifupi, mnakuja Ijumaa
Bilauzi nazo fupi, washindwa kuchuchumaa
Rukuu 'mekua fupi, 'taonesha vya kung'aa
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

6. Mtanisamehe sana, mimi kiumbe dhaifu
Nimesema niloona, moyo wangu ni dhaifu
Sitara inanikuna, nangu mipa mpofu
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

7. Msivae za kubana, mnapokua njiani
Hata kama huna bwana, usizurure mjini
Mtakuja kukumbana, usijesema kwa nini
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

8. Kimtandio kidogo, kutwa kucha kuzurura
Embu ona hilo chogo, utadhania bakora
Wala sio jambo dogo, umesahau kudura?
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

9. Shungi ndogo shingo wazi, wasema umeolewa
Hujafunzwa na wazazi, na kungwi haukupewa?
Acheni nigawe dozi, kipaji nimeshapewa
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

10. Kibanio ka Mgamia, mwenyewe waona sifa
Kwa kweli mmepania, msiige mtakufa
Matendo yenda na nia, utaipata kashifa
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

11. Unapenda vya kubana, utushitue vijana
Mwili wenyewe dubwana, haushitui ndo mana
Jiheshimu tena sana, na sijali ukinuna
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

12. Nimesema vya kutosha, wala msinichukie
Msije nikurupusha, moyo wangu 'niachie
Kila muoshwa huosha, yakinifika nilie?
Mwanamke vaa shungi, kizuri chajulikana.

Abdallah Kalindima
(CHUMA CHAKAVU)
kalindimasenior@gmail.com

Nyuki wa asali na mti

Ilikuwa wakati wa masika. Wanyama wote wa msituni walifurahi sana kwa sababu miti ilikuwa na maua mazuri na ya kushangaza. Nyuki hutoa nekta kutoka kwa maua haya na kutengeneza asali. Asali ni chakula chao cha nyuki. Kwa sababu hii nyuki pia walifurahi sana.

Siku moja nyuki walikuwa wakichuna nekta kutoka kwa maua ya miti, wakati mti wenye kiburi ukamwambia, "Kuna nini? Unakuja hapa kila wakati na kuiba nekta kutoka kwa maua yetu. Hupaswi kufanya hivyo. Unatoa nekta yetu



kama mwizi."

"Pole rafiki yangu. Hii ni kazi yetu na pia inatupa chakula. Ndiyo maana tunafanya hivyo." Nyuki asali akauambia mti.

"Wewe si rafiki yangu. Wewe ni mwizi kwangu unayeiba asali yetu bila kuuliza. Kuanzia leo hutaweza kamwe kutoa nekta ya maua kutoka kwangu." Kusema hivi, mti ulimfukuza nyuki.

Baada ya muda, mti uliitisha mkutano na masahaba wake wengine. Miti yote ya msitu ilikuwepo katika kusanyiko hilo. Mti huo ukawaambia wote, "Marafiki, leo nimewaita hapa ili kujadili jambo muhimu sana."

«Sawa, ikiwa ni hivyo, tuambie hivi karibuni.» Mti mwingine ukamwambia.

«Jambo ni kwamba nyuki wamevuka kikomo. Nyuki hao wa asali huja na kuiba nekta kutoka kwa maua yetu bila kuuliza. Wote hufanya asali zaidi kuliko lazima. Hatutawaruhusu wachukue asali yetu kuanzia leo."

Kila mtu mwingine alikubali juu ya mti huo. Pia walikataa



kutoa nekta kwa nyuki wa asali.

Siku iliyofuata kundi la nyuki liliingia msituni na miti ikatikisika mara tu ilipoanza kukaa juu ya maua. Baada ya hayo nyuki wote wakaruka. Tena wote wakaanza kukaa juu ya maua. Lakini tena miti ilitikisika kwa nguvu. Miti yote inapiga kelele juu yao na kusema, «Ondokeni ninyi nyote kutoka hapa na msije hapa. Tumeamua kwamba hatutakuruhusu kuchukua nekta yako. Ondoka hapa."

Baada ya kusikia mambo hayo yote, nyuki wote walirudi kwenye mzinga wao. Kila mmoja kwa pamoja alizungumza na malkia wao Nyuki kuhusu tatizo hili. Kila mtu alimwambia malkia wa nyuki, "Malkia, miti yote msituni imeamua kwamba kuanzia sasa na kuendelea hawataturuhusu kuchukua nekta ya maua yao. Katika hali kama hii tutakufa kwa njaa. Sasa unatuambia nini cha kufanya?»

Malkia wa Nyuki alikuwa na wasiwasi sana kusikia hivyo. Baada ya kufikiria kwa muda, alisema, "Tutaondoka kwenye msitu huu na kwenda mahali pengine ambapo tunaweza kupata asali kwa urahisi."

Kwa agizo la malkia, nyuki wote waliondoka msituni. Miti yote ilifurahi kuona nyuki wakiondoka msituni. Sasa msitu huo haukuwa na nyuki. Hakukuwa na nyuki waliobaki msituni.

Kwa sababu hii, poleni ya maua haikuweza kutoka kwa maua moja hadi nyingine. Matunda ya miti yaliacha kuja. Wala mbegu za matunda na miti mipya hazikuacha kukua msituni. Hali ya msitu ilikuwa mbaya sana. Kisha miti ikaitisha mkutano tena. Miti yote ikaanza kusemezana kwamba mbona hakuna matunda juu yake? Kwa nini maua yao hayabadiliki katika matunda?

Kisha kipepeo akawajia na kusema, "Tunapokaa kwenye maua yako na kuchukua nekta yako, basi chavua ya maua hunata kwenye miili yetu. Tulipoketi juu ya ua jingine, chavua ilihamia kwenye ua hilo. Na kwa sababu ya ua hilo kubadilishwa kuwa matunda. Hii hutokea kwa nyuki pia na wao ndio wenye uwezo zaidi wa kufanya hivi. Hawapo tena kwa hivyo poleni haisogei kutoka ua moja hadi jingine. «

Kusikia haya yote, miti iliamua wenyewe kwamba watawaita tena nyuki wa asali na kuwaacha kuchukua nekta ya maua yao. Baada ya hayo, miti ikamwambia njiwa, "Rafiki yangu inabidi uchukue ujumbe na uende kwa nyuki wa asali. Unapaswa kuwaambia kwamba miti yote katika msitu wetu inawaalika kurudi hapa na wanaweza kuchukua nekta kutoka kwa maua yetu kadri wawezavyo. Hatutawakataa."

Kuchukua habari hii, njiwa akaenda kwa nyuki na kumwambia mambo haya yote kwa malkia wa nyuki. Kusikia haya yote, malkia wa nyuki alikubali kurudi kwenye msitu huo. Malkia aliwaamuru watu wake wote warudi kwenye msitu uleule walikotoka. Waliporudi msituni, miti yote iliwaomba



msamaha na Malkia wa Nyuki akakubali msamaha wao.

Sasa nyuki hao wote wangeweza kuchukua asali kutoka kwa maua ya miti, kwa sababu hiyo miti ilianza kuzaa na mbegu zikaanza kurudi. Hii ilisababisha miti mipya kuinuka tena msituni.

Maadili ya hadithi - Hadithi hii inatufundisha kwamba hatupaswi kujipenda sana na kuwasaidia wengine. Jinsi mti ulivyojua kwamba asali ni chakula cha nyuki, lakini wanakataa kuwapa asali yao. Kwa sababu hiyo wanapaswa kukabiliana na matatizo. Kwa hivyo tunapaswa kufanya kazi nzuri kwa wengine.

Jinsi ya kupika Kashata

Na **Mtandao**



VIPIMO

1. Karanga - ½ kg
2. Sukari ya kahawia - ½ kg
3. Maji - ¼ kikombe
4. Siagi - 1 Kijiko

NAMNA YA KUPIKA KASHATA

1. Pasha sufuria jikoni kwa moto wa wastani. Zikaange karanga kwa dakika 4 - 5 kaanga hadi ziive, kuwa makini zisiungue kuwa nyeusi.

2. Zikiiva zitoe jikoni wacha zipoe toa maganda ili ziwe nyeupe.

3. Tumia moto mdogo na weka sufuria jikoni tia sukari na maji. Koroga taratibu hadi sukari na maji kuchanganyika na kunata huchukua kama dakika 6-7.

4. Mimina karanga kwenye mchanganyiko wa maji na sukari, changanya vizuri kwa dakika chache na zima jiko.

5. Pakaza sahani siagi na mimina mchanganyiko. Kisha tandaza vizuri wacha ipoe kwa dakika muda kidogo.

6. Kisha kata vipande ikiwa ya moto moto. Weka sehemu ya ubaridi ili kuganda. Baada ya hapo Kashata za karanga zitakuwa tayari kuliwa.

NB; Ni biashara nzuri sana endapo ukiweka eneo lenye wapita njia wengi au wanafunzi

KUTOKA MAKTABA

Na Ally Hamisi Mbambwa

Mbinu za Mahubiri

Licha ya jumuiya kutopata usajili hadi leo hii, lakini kuna nafuu kubwa mnoo imepatikana ya kufikisha ujumbe wa Jamaat.

kufanya mahubiri katika mji wa **Unguja - Zanzibar**, miaka ya 1990 ilikuwa ni kujitia kwenye tanuru la moto mkali huku unajiona.

Lakini, Vijana watatu, na wakati mwingine wakiwa watano, Walizunguuka katika viunga vya mji wa Unguja na vitongoji vyake wakifanya mahubiri kimya kimya bila wakazi wa mji huu kuwashitukia kwamba wanapanda mbegu mbaya ya Kikadiani kama walivyoiita.

Katika harakati zao za kufikisha ujumbe, Mmoja wao walimfanya sheikh, Alhamdulillah, kwa hakika cheo hiki walichompa zama hizo ni kama walikuwa wakifanya ubashiri. kwa fadhila za Allah leo hii anaitwa Sheikh **Abdulrahman Mohamed Ame sahib**. Mwingine alikuwa muuliza maswali magumu ya kisuni suni hususan yale yanayolenga itikadi za jumuiya, huyu alikuwa ni **Mwl Abdullah Khamis Mbanga sahib**. Na wa tatu alikuwa ni mshabiki, mwenye maswali ya nyoongeza na mtata kidogo, hapa walibadilishana, Alikuwepo **Hery Mohamed Hery sahib** , au **Amer Mohamed Heri sahib**, aidha Mwl Said Othman sahib.

Mabwana hawa walianzisha mjadala katikati ya shughuli za watu huku kila mmoja akijifanya hamjui mwenzake. Baada ya watu kujaa, shughuli ya mahubiri iliendelea bila mushkeli wowote, japokuwa itikadi ya kuendelea kwa utume na kifo cha nabii Isa a.s zilitajwa waziwazi.

Aya za Quran ziliposomwa kuthibisha madai ya utume kuendelea au Nabii Isa a.s amefariki, wapemba na waunguja walibaki vichwa chini hususan pale aya hizo zilipokuwa zikitoka kwenye kinywa cha mpemba mwanzao.

Mahubiri haya yalizaa mijadala ya hapa na pale lakini yaliacha maswali mengi kwenye vichwa vya wasikilizaji kiasi wengi waliondoka baada ya mjadala huo wakiwa na mtazamo tofauti na kile walichokuwa wanaamini au kukijua.

Mbegu ilipandwa mioyoni mwa waZanzibar wengi na miongoni mwao wakiendelea kujiunga na Jamaat, Alhamdulillah.

Mahubiri haya, yamebaki kuwa ni sehemu ya kutajwa, kutokana na hali ya uadui iliyokuwepo zama hizo dhidi ya Jamaat.

Hakika mbegu waliipanda Alhamdulillah na leo hii unaweza kufanya muhadhara hadharani, na hakuna wa kukukataza japo visununu kidogo vipo.

Allah Awalipe malipo bora kwa juhudi waliyoifanya kwa nchi hii.

Hili ni funzo kwetu. wakati tukiwa hatuna kiziwizi chochote, Tujitokeze kufanya mahubiri kwa wingi. Kwani Allah Atatuuliza.

Itaendelea Inshallah

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[as]

Hali ya Baadaye ya Ahmadiyyat

Natangaza kwa matumaini na uthabiti kwamba mimi nasimama juu ya haki na kwamba kwa fadhili za Allah, nitatokea kuwa mshindi katika harakati hizi. Kadri niwezavyo kuona kwa nuru ya macho yangu yaonayo mbali naukuta ulimwengu mzima hatimaye ukifunikizwa na hatua za maendeleo ya ukweli wangu. Wakati unawadia ambapo mimi nitapata ushindi mkubwa. Hii ni kwa sababu sauti nyingine yazungumza kwa kuunga mkono nisemayo, na upo mkono mwingine unaofanya kazi ili kuupa nguvu mkono wangu. Dunia haiuoni mkono huu, lakini mimi nauona. Nafsini mwangu yajitokeza sauti ya Dhati wa mbinguni inayolipa uzima kila neno nisemalo. Mwamko na kiherehere vimezuka juu mbinguni vimeumba kutokana na fumba la udongo kiumbe mnyonge ambaye matendo yake yanaongozewa huko juu mbinguni. Wale wote ambao, mlango wa toba bado haujafungwa kwao hivi karibuni wataona kwamba mimi si mimi binafsi. Je, yaweza kuwa macho yaonayo yasiyoweza kumtambua mtu mkweli? Je, aweza akawa hai yule ambaye haumwingii akilini wito huu wa Mbinguni?

(Roohani Khazain Jal. 3, Uk. 403: Azalae Auham sehemu II)

Jueni ya kwamba huu ni mti uliopandwa na Mkono wa Mungu. Hatauacha ukauke. Yeye Hatatosheka mpaka pale atakapouona umestawi na kufikia kima chake. Atahakikisha kwamba umemwagiliwa maji ya kutosha naye Atauzungushia ugo kuulinda. Hivyo Mwenyezi Mungu Atawabariki wafuasi wangu kwa mafanikio ya ajabu na ustawi. Je, hamkufanya chini juu kuupinga? Lau kama hii ingelikuwa kazi ya mwanadamu, mti huu ungelikuwa tayari umesha katwa na kuangushwa kitambo sana na haingebaki alama yake hata chembe.

(Roohani Khazain Jal. 11, Uk. 46, Anjam-e-Atham)

MATUKIO KATIKA PICHA




Kambi ya Malezi siku 5 Simiyu




Mh Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania alishiriki mahafali ya wahitimu wa darasa la 7 wa shule ya awali na msingi ya Ahmadiyya iliyopo Morogoro




Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania ukiongozwa na Mhe Amir na Mbashiri mkuu wa ulitembelea Bunge la Tanzania




Mhe Amir na mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania pamoja na wajumbe walionana na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)1




Mhe. Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania pamoja na wajumbe walionana na Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)




Sheikh wa Mkoa Dar es Salam alionana na Mkuu wa wilaya Ilala Mhe. Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija alipomtembelea ofisini kwake




Mhe. Sh Tahir Mahmood Chaudhary Amir na Mbashiri mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania pamoja na wajumbe walionana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Dodoma




Wajumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania wakiongozwa na Mhe Amir na mbashiri mkuu walitembelea ofisi ya Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)







Matukio mbalimbali katika Ijtimaa ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania 2022

Ustadh Aapa Akishika Qur-An Bila Yakini



Hassan Sango
Mwandishi wa makala hii

Tukio hili lilitokea siku chache baada ya mmoja katika ya washirika wake mpemba aitwaye Ismail Idarus ambaye kwa muda mrefu amekuwa mpinzani wa Ahmadiyya bila ya ushidi wa kutosha na unapotaka kuongea ili umfahamishe husema huwezi elewa dini kwa Kiswahili. Pia huniambia sijui kiarabu wala kusoma Qur'an kwa ufasaha .

Niliamua kumuahidi kwamba tufanye mjadala akinishinda nitampa 100,000/= na yeye nikimshinda atanipa kitu akawa anakwepa, kwa fadhila za Mwenyezi Mungu siku hiyo nilikuwa nasikiliza ushaidi wa BBC toka kwenye flashi kuwa Yesu hakufa msalabani bali alihamia Kashmir na akafia huko.

Bwana Mpemba baada ya kusikia sehemu yake akasema hakusikia AYA ya Qur'an wala hadithi kwa maana ya kudharau kilichoelezwa, kwa sababu ni muda mrefu alikuwa anasumbua nilimwambia kuwa nina shilingi 10,000/= ambayo niliitoa na kumkabidhi muuza vinywaji aliyekuwa karibu yetu ni kamwambia bwana Mpemba leo tufaidike ukinishinda chukua hicho kiasi cha fedha, akakubali nay eye akasema kwamba lazima nianze kuonge mimi, binafsi nikamwambia kuwamba anza wewe unayenishtumu na kiukweli sitaingilia mazungumzo yako na wewe ikifika zamu yangu utulie.

Ndipo alipoanza kuwasilisha kwa kusema “wama swalabuhu wamaqatluhu bal rafaa allahu ziah “ yaani hawakumua wala hawakumsulubisha bali mungu alimnyanyua kwake. Swali linakuja kwenu nyinyi Ahmadiyya kwanini mnadai kuwa amekufa wakati Qur'an yakanusha.

Bwana Mpemba kwa hakika hakuchukua muda mrefu kuongea na ilipofika zamu yangu nikasema Allahmdolillah nakushukuru sana ndugu yangu uliposema Isa (A.S) amepaa ulikwisha kili kuwa amekufa kwa sababu Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an tayar alishamuahidi nabii ISA (A.S) atamnyanyua baada ya kumfisha, nikamsomea ahadi kwa kiarabu na kutoa tafsiri sura (3:56) ya kwamba “***kumbukeni mwenyezi mungu aliposema ewe Isa kwa yakini mimi nitakufisha na kukuinua kwangu***” hivyo basi a ahadi ya mungu ilikuwa ni kumuinua baada ya kumfisha hivyo kusema kwako amepaa ni kukiri kifo chake hapo akachanganyikiwa akaenda kuleta Qur'an akitaka nimsomea hivyo nikasoma nakutoa tafsri na kumwambia kwamba kama unapinga lete aya ambayo inayosema kwamba alimpaisha kabla hajamfisha kiukweli hakuipata. Pembeni alikuwepo mkristo mmoja ambaye na yeye alikuwa anasikiliza mazungumzo yetu, mkristo yule akasema kwa muda mfupi nilivyosiikiliza mazungumzo yenu mzee wangu umeshinda maana bwana mpemba yeye hajibu hoja bali anazunguka tu, nikaondoka nikiwa na ushindi na baadaye tulipokutana akasema alete maneno ya wanazuoni nikakataa.

Hata leo wakati sijaanza kuandika Makala kurejea usemi wake huo mimi nimefahamisha kama zilivyo sharia za nchi kwa maana ya katiba ndio sharia kuu, hivyo basi sheria yeyote mtakayo tunga ikipingana na katiba hiyo sheria ni batili, swali je maneno ya wanazuoni yapinganayo hayatakuwa BATILI hiyo ndio sababu nayakataa.

Kuhusu Tukio la Ustadhi Kushika Qur'an na Kuapa Hilo Lilikuja Ghafla

Ustadh huyo anaitwa Ismail Idarus.

Baada ya mimi kumaliza sala pale ustadhi Ismaili Idarus ambaye ni imam wa msikiti huo alikuwa ameketi na wafuasi wake kadhaa na kama kawaida yake aliponiona alitamka maneno ya dharau kama moja ya meneno aliyoyasema ni kwamba “waahmadiyya wanadai unabii hawana ushahidi, kwa sababu wanasema ISA akija atakuwa nabii wakati unabii baada ya Muhammad hakuna” akanitaka nitoe ushahidi nikwambia ISA ametajwa mara 4 katika hadithi moja kwamba akija atakuwa nabii hapo nilisahau hiyo hadithii ndio maana nikasema hivyo katika Bukhari baada ya Muslim nilikuwa nimeahidi kumpatia ushahidi baada ya kushika QUR'AN na kusema mungu aepushie mbali wazo hili Ahmad Mirza sio nabii sikuona umuhimu tena baada ya siku kadhaa aliponiona akaniambia wale waliokuwepo siku ile bado wanasubiri ushahidi hivyo nikamwambia ISA kaitwa Nabii mara 4 katika Muslim pindi atakapo rudi.

Nilielezakuwakilasikutunaposali tunaomba kuwa tuongozwe katika njia iliyonyooka, njia ya wale aliyowaneemesha Mwenyezi Mungu amabo wametajwa katika sura ya 4:70 na si wengine ni manabii, masadiq, mashahidi na masalih hapo kasema neno MA’A haliwezi kuwa miongo hivyo ilinibidi nimpe ushahidi toka kwenye Qur'an tukufu sura (3:194) tunapoomba Mungu atufishe tukiwa miongoni mwa wema na AYA 146 hadi 147 ambazo zinasema kwamba wanafiki baada ya kutubu watakuwa miongoni mwa waaminiobaada ya kukata tafsri hiyo alitoa muongozo kuhusu neno MA’A analeta maelezo bila ya AYA, lakini chakusikitisha sana baada ya kujibu hoja akatoa Qur'an nakuapa .

Hawa ndugu zetu wanathibitsha ukweli wa Qur'an ni sura (2:258) Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini na huwatoa katika giza na kuwapeleka katika muangaza lakini waliokufuru walizi wao ni mashetwani huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza kwenye giza, hao ndio watu wa motoni na humo watakaa sura hiyo ni 2:15 wanafiki kwa kuwa fuata wakubwa hukawa na imani ya kweli ambayo ndio nuru.

Hivyo Ustadhii Ismaili kusudio lake limekuwa niache Qur'an ambayo nuru isemayo Waislam watakao mtii Mtume (saw) watapata vyeo 4 yaani Unabii, Usadiq, Ushahidi na Usalih.

Niende kwenye giza la masheikh wake ambao wamekataa neema ya unabii bila ya dalili yoyote iliyowafikia na hao Mungu amewaita kuwa ni chukizo kubwa mbele yake na mbele ya waaminio, hatari zaidi soma sura 40:35-36.

Hivyo kama Ustadhi Ismaili na watu wenye itikadi kama yake wanataka radhi za Mwenyezi Mungu tiba ya kweli kuwa ni Masihi Mirza Ghulam Ahmad ambaye alifunuliwa ufunuo huu *“mimi nitamfedhesha kila ataayekufedhehesha”*.

Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu mola wa walimwengu.

Ijtimaa Ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Yafana.

Na Isihak Nyamihasi
M.K.A Tanzania

Tanzim ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, imefanikiwa kufanya mkutano wake wa mwaka wa 32 katika viwanja vya Ahmadiyya Kitonga Dar es Salaam.

Mkutano huo wa mwaka 2022 ulianza siku ya Ijumaa ya 5 Agosti hadi jumapili 7 Agosti mwaka huu,ikiwa na kauli mbiu ya Quran na Tajwid huku wahudhuriaji 534 kutoka nchini kote wakishiriki Ijtimaa hiyo. Katika jumla hiyo ya wahudhuriaji, Khuddam walikuwa 342 huku Atfal walikuwa 192 ikijumuisha Waalimu, Mashekh na wageni mbalimbali kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Kwa fadhili za Allah, Ijitimaa hiyo ilifungamana na mkutano wa mwaka wa Jalsa Salana ya Uingereza, hivyo kutoa fursa kwa wahudhuriaji kufatilia kwa ukaribu hotuba mbalimbali za Khalifa mtukufu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a), na mwisho wahudhuriaji walishiriki baiati ya pamoja (International Baiat) kwa mkono wa Khalifa kupitia channel za MTA Afrika.

Katika siku zote tatu za mkutano huo, wahudhuriaji walipata fursa ya kushiriki katika matukio kadhaa ikiwa ni pamoja na hotuba mbalimbali, mashindano ya kielimu na michezo iliyoshirikisha Khuddam na Atfal wote waliohudhuria na zawadi mbalimbali zilitolewa kwa washindi wa mashindano hayo, huku wakila na kunywa kwa pamoja katika muda wote wa Ijtimaa.

Katika kufanikisha mkutano huo, Majlis khuddamul Ahmadiyya Tanzania iliweza kuandaa maonyesho kadhaa yaliyolenga kutoa elimu kwa wahudhuriaji yakiambatanisha vitabu mbalimbali vya Jamaat, mabango yenye jumbe kadhaa kwa wasomaji, mavazi ya sare za tanzim n.k, hakika ijitimaa ilifana sanam Alhamdulillah.

Makhalifa Walioongoka

Hadhrat Abu Bakr*ra*

Kutoka uk. 12

ambayo Hadhrat Abu Bakr*ra* aliikusanya katika jalada moja kupitia kwa Hadhrat Zaid bin Thabit inaitwa Sahifah Siddiqi. Hiyo ikabaki kwa Hadhrat Abu Bakr*ra*, kisha kwa Hadhrat Umar*ra*, na kisha kwa Ummul-Mouminin Hadhrat Hafsah binti Umar*ra*. Hadhrat Uthman*ra* alitengeneza baadhi ya nakala za muswada huu na kisha akaurudisha kwa Hadhrat Hafsah. Wakati Marwān alipokuwa mtawala wa Madina mwaka wa 54 Hijria, alitaka kuchukua hati hii kutoka kwa Hadhrat Hafsah lakini alikataa kumpa. Baada ya kufariki Hadhrat Hafsah, Marwān aliichukua nakala hii kutoka kwa Hadhrat Abdullah bin Umar*ra* na kuiharibu.

Hadhrat Ali*ra* anasema kwamba Hadhrat Abu Bakr*ra* alikuwa wa kwanza kuhifadhi Qur'ani Tukufu katika muundo wa kitabu.

Hadhrat Muslih Maud*ra* anasema: Ukweli ni kwamba hakuna maandishi yoyote duniani ambayo yamehifadhiwa mfululizo kama Qur'ani Tukufu. Wakati wa Mtukufu Mtume*saw*, Qur'an yote ilikuwa imeandikwa, lakini haikuwa imekusanywa katika jalada moja. Kwa hiyo, Hadhrat Abu Bakr*ra* aliamuru 'ikusanywe' na sio 'iandikwe'. Maneno yenyewe yanaweka wazi kwamba lilikuwa ni suala la kukusanya Qur'ani Tukufu, sio kuiandika. Wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat Uthman*ra* kutoka katika usomaji mbalimbali wa Qur'ani Tukufu, ulimwengu wa Kiislamu ulikubaliana lahaja moja ya Kiquraishi. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba Khalifa wa kwanza, Hadhrat Abu Bakr*ra*, alikusanya sura zote za Qur'ani Tukufu kulingana na amri aliyoisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume*saw*. Baada ya Hadhrat Abu Bakr*ra*, Mwenyezi Mungu alimwezesha Hadhrat 'Uthman*ra*, Khalifa wa tatu, kukusanya Qur'ani Tukufu iliyokuwa inaafikiana na lahaja ya Maquraishi na kuieneza ndani ya nchi zingine.

Sifa alizokuwa nazo Hadhrat Abu Bakr*ra* zinaitwa Awwaliāt-e-Abu Bakr. (yaani kuwa wa kwanza kwa Abu Bakr). Nazo ni kama zifuatazo:

Alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu. Alikuwa wa kwanza kujenga msikiti mbele ya nyumba yake huko Makka. Alikuwa wa kwanza kupigana na makafiri wa Makka, kwa kumuunga mkono Mtukufu Mtume*saw*. Alikuwa wa kwanza kununua uhuru kwa watumwa (wanawake na wanaume) waliokuwa wakiteswa kwa ajili ya Uislamu. Alikuwa wa kwanza kukusanya Qur'ani Tukufu katika jalada moja. Alikuwa wa kwanza kuitaja Qur'an Tukufu 'Mas'haf'. Alikuwa Khalifa wa kwanza wa Mtukufu Mtume*saw*. Aliteuliwa kuwa Amīr-e-Hajj wa kwanza wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume*saw*. Aliwaongoza Waislamu katika sala kwa mara ya kwanza wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume*saw*. Alikuwa wa kwanza kuanzisha Baitul-Māl katika Uislamu. Alikuwa ndiye Khalifa wa kwanza ambaye Waislamu walimwekea posho. Alikuwa Khalifa wa kwanza kumteua mrithi wake. Alikuwa ni Khalifa ambaye baba yake alikuwa bado yu hai wakati alipopokea Bai'at kama Khalifa. Alikuwa mtu wa kwanza katika Uislamu ambaye Mtukufu Mtume*saw* alimpa cheo. Alikuwa ni mtu ambaye vizazi vinne vinavyoungana naye vilikuwa na heshima ya kuwa masahaba wa Mtukufu Mtume*saw*.

Hadhrat Aisha*ra* anaelezea sura ya Hadhrat Abu Bakr*ra* kama ifuatavyo: Alikuwa na ngozi nyeupe na mwembamba. Alikuwa na nyama ndogo kwenye mashavu yake. Mgongo wake ulikuwa umepinda. Macho yake yalikuwa yamezama sana, na paji la uso wake lilikuwa juu.

Hadhrat Anas*ra* anasimulia kwamba Hadhrat Abu Bakr*ra* alikuwa akipaka rangi kwenye nywele zake. Siku moja, Hadhrat Abu Bakr*ra* alipomwona ndege, alisema: Laiti ningekuwa kama ndege huyo, kwani hataulizwa wala kuwajibishwa.

Wakati wa kufariki kwake, Hadhrat Abu Bakr*ra* alimwambia Hadhrat Aisha*ra*: Ewe binti yangu! Unajua kuwa wewe ndiye mpendwa zaidi kwangu na nilikupa zawadi ya kipande fulani cha ardhi, lakini hukukimilikisha kwako. Sasa, nataka uirejeshe ardhi hiyo ili igawanywe miongoni mwa watoto wangu wote kwa mujibu wa sheria zilizowekwa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, ili niweze kusema mbele ya Mungu kwamba sikumpendelea mtoto wangu yeyote kuliko wengine.

Siku moja baada ya kufanywa kuwa Khalifa, Hadhrat Abu Bakr*ra* alikuwa akienda sokoni akiwa amebeba jora la kitambaa mabegani mwake ili aweze kukiuza na kutafuta riziki kwa ajili ya familia yake. Akiwa njiani, alikutana na Hadhrat Abu Ubaidah na Hadhrat Umar*ra* ambao kwa ushauri wao alitengewa malipo. Pesa hiyo ilikuwa nini? Alipewa usafiri kwa ajili ya safari zake na gharama zake sawa na zile alizotumia kabla ya kuwa Khalifa na shuka mbili, ambazo zikizeeka zingebadilishwa kwa mpya.

Hadhrat Muslih Maud*ra* anasema kwamba Hadhrat Abu Bakr*ra* alikuwa mtawala wa ulimwengu wote wa Kiislamu, lakini hakupata malipo yoyote. Alikuwa mlinzi wa mali za watu lakini hakuzitumia kwa ajili yake mwenyewe. Kama hatamu ingeanguka mikononi mwake, angeshuka kutoka juu ya ngamia na kuiokota yeye mwenyewe. Alipoulizwa kwa nini hakumwomba mtu mwingine amkabidhi, alisema kwamba alikuwa ameamrishwa na kipenzi chake Mtukufu Mtume*saw* asimuombe yeyote kitu chochote.

Mtukufu Mtume*saw* siku moja alisikia watu wakisema, ubora wa Abu Bakr ni upi juu yetu? Yeye husali tunavyosali na kufunga vile tufungavyo. Mtukufu Mtume*saw* akasema, ubora wa Abu Bakr hautokani na sala na saumu yake. Ni kwa sababu ya wema ulio moyoni mwake.

Akielezea hadhi ya juu ya Hadhrat Abu Bakr*ra*, Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake) anasema: Maisha ya pili ni yale ambayo Masufi wanayaita 'baqa' (kubaki na Mungu). Mtu anapofikia hatua hii, roho ya Mwenyezi Mungu hupuliziwa ndani yake, na Malaika huteremka juu yake. Kwa hiyo, Mtukufu Mtume*saw* alisema kuhusu Hadhrat Abu Bakr*ra*, kama mtu yeyote anataka kuwaona wafu wakitembea juu ya ardhi, amtazame Abu Bakr. Hadhi ya Abu Bakr haitokani na matendo yake ya nje bali juu ya kile kilicho moyoni mwake.

Tukio lifuatalo linadhihirisha utiifu kamili wa Hadhrat Abu Bakr*ra*, upendo na heshima kwa utukufu wa Mtukufu Mtume*saw*. Siku moja alikuja nyumbani kwa Mtukufu Mtume*saw* na akamkuta Hadhrat Aisha*ra* akizungumza na Mtukufu Mtume*saw* kwa sauti kubwa. Alipoona hivyo, alikasirika na alikuwa karibu kumpiga binti yake wakati Mtukufu Mtume*saw* alipoingilia kati. Hadhrat Abu Bakr*ra* alipoondoka, Mtukufu Mtume*saw* alimwambia Hadhrat Aisha*ra* kwa mzaha, tazama jinsi nilivyokuokoa kutoka kwa baba yako leo. Siku chache baadaye Hadhrat Abu Bakr*ra* alikuja tena na Hadhrat Aisha*ra* alikuwa anazungumza kwa furaha na Mtukufu Mtume*saw*. Alipoona hivyo, Hadhrat Abu Bakr*ra* akasema, ulinifanya kuwa sehemu ya ugomvi wako, je sasa utanishirikisha furaha yako? Kusikia haya, Mtukufu Mtume*saw* alisema, tunashiriki sote.

Mwishoni mwa khutba, Hadhrat Khalifatul-Masih V*atba* alisema kwamba ataendelea na masimulizi haya katika siku zijazo, Insha'Allah.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SAF.-RAB.I 1444 AH | OKTOBA 2022 | NUBUWWAT 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Mtume^{saw}. akasema, Mtu anayewafunza binti zake adabu njema na kuwapa malezi mema, mtu huyo ataingia Peponi (Bukhari na Muslim).

Jalsa Salana Uingereza 2022

Baraka, Shukrani na Maombi

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 16/09/2022; baada ya kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano^{atba} aliendelea na mfululizo wa khutba kuhusu Hadhrat Abu Bakr^{ra}.

Hadhrat Khalifatul-Masih V^{atba} alisema: Kuhusiana na mafanikio ya Ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakr^{ra}, leo nitaelezea baadhi ya maelezo kuhusu haki za Dhimmi. Neno Dhimmī linarejelea watu waliokubali utawala wa Kiislamu huku wakiendelea kufuata dini zao wenyewe, na Waislamu walichukua jukumu la kuwalinda. Watu hawa waliondolewa kwenye utumishi wa kijeshi na malipo ya Zakat. Hata hivyo, dirham nne zilipokelewa kila mwaka kama Jizya kutoka kwa kila mtu mzima, mwenye afya njema na mwenye uwezo miongoni mwao. Wazee, walemavu, maskini, na watoto walisamehewa kutokana na hili na badala yake walisaidiwa kupitia Baitul-Māl. Wakati wa ushindi wa Iraq na Syria, watu wengi wasio Waislamu walikuja kuwa Dhimmi baada ya kukubali kulipa Jizya. Mikataba iliyofanywa nao ilijumuisha masharti kwamba nyumba zao za watawa na makanisa yasingebomolewa, wala ngome zao zozote zisingeharibiwa ili waweze kubaki wakiwa na ngome dhidi ya adui wakati wa shida. Hawangezuiliwa kupiga kengele au kuandamana na msalaba wakati wa sherehe zao.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Moja ya mafanikio makubwa na yasiyo na kifani ya Ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakr^{ra} ilikuwa ni ukusanyaji wa Qur'ani Tukufu. Wakati masahaba wapatao mia saba, ambao walikuwa wameihifadhi Qur'ani Tukufu yote moyoni, walipouawa kishahidi katika vita vya Yamaamah, Mwenyezi Mungu alimvuvia Hadhrat' Umar^{ra} kuikusanya Qur'an Tukufu katika jalada moja. Kwa mujibu wa maelezo yaliyoandikwa katika Sahihul-Bukhari, baada ya vita vya Yamaamah, Hadhrat Abu Bakr^{ra} alimwita Hadhrat Zaid bin Thabit^{ra} na kumwambia kwamba Hadhrat Umar^{ra} alikuwa amependekeza kuwa Kurani Tukufu ikusanywe, na hivyo aliikabidhi kazi hii kwa Hadhrat Zaid bin Thabit. Hadhrat Zaid bin Thabit anasema: Wallahi! Lau Hadhrat Abu Bakr^{ra} angeniamuru nihamishe mlima kutoka sehemu moja kwenda nyingine, ingekuwa rahisi kwangu. Hadhrat Zaid bin Thabit anasema: "Nimeikusanya Qur'an kutoka kwenye matawi ya mitende, kutoka kwenye mawe meupe, na kutoka kwenye vifua vya watu. Qur'an

Endelea uk 11

KITABU KIPYA

Wasifu wa Nabii Mtukufu^{saw}



Shamaa'il-un-Nabi, kitabu cha kipekee cha Imam Tirmidhi (209-279 AH) kinajikita katika sifa za kimaumbile, tabia, amali na sifa za Mtume mtukufu wa Islamu^{saw}. Vipengele hivi vya maisha ya Mtukufu Mtume^{saw} vimesimuliwa na masahaba wake mashuhuri sana^{ra}. Ni mkusanyo wa Hadith sahihi zinazojumuisha sura hamsini na sita, ambazo huhudumu kama mfano kwa wanadamu wote kufuata.

Jipatie nakala yako kwa bei ya Tsh 4,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com